# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL 7

# KISWAHILI PAPER 1 ANSWERS

1. 1. Kichwa (Anwani ya ripoti)
(a) Kichwa cha ripoti kiteuliwe kulingana na mada inayohusika. Kitaje mada, tarehe na kionekane kuwa ni kichwa cha ripoti.
(b) Kichwa kiandikwe kwa herufi kubwa na kipigiwe mstari.
2. Utangulizi
Katika utangulizi, mtahiniwa anaweza kutoa maelezo ya jumla kuhusu mada ya rupoti.
3. Ripoti(mwili)
(a) Sehemu hii iwe na vichwa vidogovidogo kuhusu mambo mbalimbali.Viandikwe kwa mpangilio mzuri wa aya na taarifa zote zipangwe kwa mtiririko mzuri.Mtahiniwa atoe taarifa kuhusu mambo aliyoyaona au kuyasikia.
(b) Habari za ripoti ziwe za kuaminika,za kweli na zielezwe kinaganaga zikiambatana na ufafanunuzi toshelevu.
(c) Nafsi ya kwanza isitumiwe katika uandishi wa ripoti.
Mtahiniwa atumie nafsi ya tatu, ripoti iandikwe kwa wakati uliopita
4. Mtahiniwa ajikite katika mada.Ataje shida kama:
(a) Umaskini unaosababisha ukosefu wa karo au sare za shule na mahitaji mengine ya masomo kama vile vitabu.
(b) Migomo ya walimu
(c) Migogoro na migomo shuleni
(d) Ndoa za lazima
(e) Ndoa za mapema
(f) Utamaduni na mila,mfano ukeketaji wa wasichana
(g) Mikasa ya moto
(h) Uavyaji wa mimba
(i) Kupigwa na baadhi ya walimu
(j) Mihadarati/madawa ya kulevya
(k) Uhusiano wa kimapenzi miongoni mwa wanafunzi
(l) Uongozi mbaya shuleni
(m) Sayansi na teknolojia-mitandao na simu tamba
Mtahini akadiriwe hoja zingine za mtahiniwa.Mtahiniwa atoe hoja tano na zaidi ndiposa awe

ametimiza maudhui.
5. Mapendekezo
Mtahiniwa anaweza kutoa ushauri na mapendekezo kuhusu taarifa aliyoishughulikia kwa kuagiza mambo ya kufanywa ama kukataza yasiyofaa kufanywa na hatua za kuchukuliwa
6. Hitimisho
(a) Katika sehemu hii,mtahiniwa aeleze japo kwa ufupi mambo muhimu katika ripoti
(b) Mtahiniwa ahitimishe ripoti kwa:
(i) Ripoti hii imeandikwa na….
(ii) Sahihi
(iii) Jina
(iv) Cheo chake
7. Mambo ya kuzingatia katika swali hili
(a) Mtahiniwa atakayekosa kuandika sura ya ripoti aondolewe alama 45(sura) baada ya kusahihisha na kuiweka insha katika kiwango chake.
(b) (i) Mtahiniwa atakayedokeza maudhui chini ya matano asipite kiwango cha C+ 09/20

(ii) Mtahiniwa ajihusishe katika kisa la sivyo amejitungia swali awekwe katika kiwango cha D- 01/20 bakshishi
(c) Mtahiniwa atakayekosa kabisa kudokeza maudhui kulingana na mada aondolewe

4 M(maudhui)baada ya kusahihisha insha na kuiweka katika kiwango chake
2. 2 Njia mbalimbali za kukabiliana na gharama ya juu ya maisha
(a) Kupunguza kudorora kwa thamani ya fedha dhidi ya fedha za kigeni kwa mfano,Dola,pauni na kadhalika
(b) Benki zihimizwe kupunguza faida zinazotozwa mikopo inayochukuliwa na wananchi wahimizwe wachukuwe mikopo inayochukuliwa na wananchi wahimizwe wachukue mikopo na kuwekeza katika nchi zao.
(c) Serikali zipunguze gharama ya matumizi ya fedha za umma
(d) Kudhibiti bei ya bidhaa
(e) Serikali ziongeze wafanyakazi mishahara kulingana na viwango vya maisha.
(f) Serikali ziwahimize wananchi kuzipa kipau- mbele bidhaa zinazotengenezwa nchini kuliko za nje,mfano vyakula,mbolea na hata vyuma.
(g) Kuweka mikakati ya kuboresha miundo msingi kama vile barabara na reli ili kupunguza gharama za kusafirisha bidhaa sokoni na viwandani.
(h) Kujenga na kufufua viwanda katika sehemu mbalimbali hasa mashinani ili wananchi wengi

waajiriwe kazi.

Mtihani akadirie hoja zingine za mtahiniwa.Mtahiniwa atoe hoja tano na zaidi ili awe amejitosheleza kimaudhui.
Mambo ya kuzingatia katika swali hili
(a) Hili ni swali la hoja
(b) Njia ambazo zinaweza kutumiwa- ni njia ambazo bado hazijatumiwa.Mtahiniwa akieleza njia ambazo tayari zimetumiwa kukabiliana na gharama ya juu ya maisha katika nchi zinazoendelea,atakuwa amejitungia swali hivyo moja kwa moja aweke katika kiwango cha D- 01/20(Bakshishi)

(c) Nchi zinazoendelea-ni nchi ambazo hazijapiga hatua kimaendeleo, mfano viwanda na ni wakati huu ambapo zinajizatiti kujiimarisha kiuchumi.
(d) Mtahiniwa ataje hoja na kuifafanua ili apewe mkwaju kamili wa alama .Akitaja hoja na asiifafanue,apewe nusu mkaju wa alama
3. 3 Sihadaike na rangi tamu ya chai ni sukari
(a) Maana ya methali-Usidanganyike na sura ya kitu au mtu.Uzuri wake umo katika tabia au matendo yake.
(b) Matumizi ya methali-Hutumiwa kumkanya mtu asipumbazike au asivutwe na sifa za nje za kitu au mtu achunguze kitu hicho au mtu huyo kwa ndani.
Mambo ya kuzingatia katika swali hili
(a) Methali zina sehemu mbili,ya kwanza na ya pili.
Mtahiniwa ashughulikie sehemu zote mbili.Akishughulikia sehemu moja atakuwa amejibu swali nusu hivyo asipite kiwango cha C alama 08/20
(b) Mtahiniwa achague kisa au visa vinavyoafikiana na methali.
(c) Lazima kisa kiwe na pande mbili yaani:-
(i) Sihadaike na rangi-mtu anapumbazika na kuvutiwa na sifa za nje za kitu au mtu
(ii) Tamu ya chai ni sukari-yaani amekosa uzuri aliotarajia kupata kutoka kwa kitu au mtu huyo
(d) Katika kisa cha mtahiniwa,sehemu ya kwanza au mwanzo tuone mtu anapumbazika na Kuvutiwa na sifa za nje za kitu au mtu.Sehemu ya pili au mwisho mtu huyo anakosa uzuri aliotarajia kupata kutoka kwa kitu au mtu huyo.
(e) Insha iwe na utangulizi bayana mwili au yaliyomo na hitimisho mwafaka lenye kuleta nasaha au funzo.
(f) Methali hii isipingwe na mtahiniwa.Akiipinga asipite kiwango cha D.
(g) Mtahiniwa akiandika kisa au visa ambavyo havioani na methali hii,amejitungia swali hivyo awekwe katika kiwango cha D- 01/20 (Bakshishi)
4. Mambo ya kuzingatia katika swali hili
a) Hii ni insha ya mdokezo
b) Kisa kiwe cha kusisimua na kionyenhe furaha na kushangilia kwa vifijo na nderemo shuleni
c) Ushindi ndio uwe mara ya kwanza kupatikana na unaweza kuwa unahusu mambo yafuatayo (i)Ushindi katika mtihani wa kitaifa
(ii) Michezo ya kuigiza
(iii) Nyimbo au ngoma,mashairi, riadha, mpira na kadhalika
(d) Mtahiniwa atamatishe insha kwa kufunga alichopewa la sivyo atakuwa amejitungia swali na kulijibu hivyo apewe bakshishi D- 01/20
(e) Atunge kisa ambacho kinaoana na kifungu alichopewa.
(f) Mtahiniwa aonyeshe ni wale waliokuwa shuleni mwake waliofurahi na Na kushangilia wala si watu wengine. Akionyesha ni watu wengine nje ya shule atakuwa amejitungia Swali,awekwe katika kiwango cha D- 01/20(bakshishi)
(g) Anayeongeza maneno mawili hadi matano katika kifungu alichopewa Aondolewe maki 2 Z(ziada)baada ya kusahihisha na kuiwekainsha katika Kiwango chake.
(h) Mtahiniwa akiongeza zaidi ya maneno matano katika kifungu alichopewa, Atakuwa amejitungia swali hivyo awekwe katika kiwango cha D-01/20 (bakshishi)
(i) Mtahiniwa akikata maneno mawili yasiyoathiri mada,asichukuliwe kuwa Amejitungia swali
(j) Akiacha sehemu muhimu ya kifungu,amejitungia swali,apewe bakshishi